JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**
**SHAURI NA. 03 - 2019/2020**

# LEMUTUZ ONLINE TV

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa Lemutuz Online TV, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Mnamo tarehe 10 Agosti, 2019, Lemutuz Online TV kupitia chaneli yao walionesha kwa uwazi miili ya watu waliofariki dunia baada ya kuungua vibaya kwa moto katika ajali ya gari la mafuta iliyotokea Msamvu mjini Morogoro bila kuzingatia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018 na maadili ya uandishi wa habari. Maneno yafuatayo yalisikika kutoka Lemutuz Online TV wakati picha za miili ya watu waliofariki dunia ikioneshwa kwa uwazi;

*"...Watu wanaungua!!!...watu wanaungua msamvu!!!, ni ajali kubwa ya moto, watu wanaungua, watu wanaungua, watu wanaungua msamvu, watu wamekufa, ni moto Msamvu stendi, Msamvu stendi..."*

1.4 Lemutuz Online TV ilirusha picha za watu waliofariki dunia katika ajali bila kuzingatia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018 ambazo zinamtaka mmiliki wa mtandao azingatie weledi na maadili ya uandishi wa habari katika kuweka maudhui mtandaoni na kuhakikisha maudhui yake hayaleti usumbufu wa kisaikolojia kwa watazamaji wake au kusababisha woga/wasi wasi. Vile vile, kutoweka au kuonyesha kwa uwazi picha za majeruhi waliopata ajali au miili ya watu waliofariki dunia kwa ajali, au picha za watu waliouawa katika vita, machafuko au maafa.

1.5 Kitendo cha kuweka picha hizo, Lemutuz Online TV imekiuka Kanuni Na. 7 (1) (a) (b) na 12 (f), (h) (g) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

7(1) *A licence of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining and educating the public shall adhere to the following conditions:*

*(a) content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;*

*(b) adhere to journalism ethics and professionalism;*

*12. Online content services provider shall not publish;*

*(f) content that portrays violence, whether physical, verbal or psychological; that can upset, alarm and offend viewers and cause undue fear among the audience or encourage imitation;*

*(g) content that portrays sadistic practices and torture, explicit and excessive imageries of injury and aggression, and of blood or scenes of executions or of people clearly being killed;*

*(h) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder.*

## 2.0 WITO WA KUFIKA MBELE YA KAMATI YA MAUDHUI

Tarehe 23 Agosti, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Lemutuz Online TV,** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 28 Agosti, 2019, saa 04:00 asubuhi, uongozi wa Lemutuz Online TV ukiongozwa na Bw. William Malecela, Mmiliki na Mkurugenzi Mtendaji wa Lemutuz Online TV aliyeambatana na David Phinisony, Mwandishi wa Lemutuz Online TV, ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria kwa tuhuma zinazowakabili.

## 3.0 KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI MTANDAONI YA LEMUTUZ ONLINE TV

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Lemutuz Online TV** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 10 Agosti, 2019 yaliyochapishwa na Lemutuz Online TV katika chaneli yao mtandaoni ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 4.0 MAELEZO YA UTETEZI YA LEMUTUZ ONLINE TV

Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa **Lemutuz Online TV** umeomba radhi kwa kosa walilolifanya na usumbufu uliojitokeza wakidai kwamba kosa hilo lilisababishwa na uzembe wa msimamizi wao wa maudhui ambaye hakutumia busara na kuzingatia weledi katika uchapishaji wa video ile. Waliomba wasamehewe kwa kosa walilolifanya a kwa kuzingatia ni kosa lao la kwanza. Waliahidi kutorudia kosa na pia kuahidi kuongeza ufanisi katika uandaaji, uchakataji, na usambazaji wa taarifa zao kwa jamii.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **Lemutuz Online TV** waliendelea kueleza yafuatayo;

4.1 **Bw. William Malecela** ambaye ni Mmiliki na Mkurugenzi Mtendaji wa Lemutuz Online TV alikiri kosa na kujitetea kuwa siku ya tukio alikuwa hospitali akitibiwa, na alipotoka hospitali alikwenda moja kwa moja TBC kuhamasisha watu wasichapishe picha na video za majeruhi na marehemu wa ajali ile mitandaoni bila ya kujua kwamba picha na video zile zimechapishwa kwenye mtandao wake pia. Alidai kuwa kosa hilo lilisababishwa na uzembe wa msimamizi wake aliyemuachia ofisi, Bw.Joseph Joseph na hata mwandishi aliyechapisha alipoulizwa, alijibu kuwa hakuelewa kama lile ni kosa na aliona mitandao mingine ikichapisha pia. Alisema kuwa ameshamfukuza kazi msimamizi wake huyo mzembe kwa barua na aliikabidhi Kamati nakala ya barua hiyo.

Aliendelea kusema kuwa yeye kama yeye amekuwa mstari wa mbele kuihamasisha jamii kuhusu jitihada mbali mbali za Serikali. Alimalizia kwa kuomba radhi na kusema kuwa hili ni kosa lao la kwanza tangu chaneli yao ilipoanzishwa mwaka 2012 na kwamba picha na video zile zimeshaondolewa katika chaneli yao.

## 5.0 MAJUMUISHO YA UTETEZI WA LEMUTUZ ONLINE TV

Katika kujumuisha utetezi wao, Bw. **William Malecela** aliendelea kuomba radhi na kusema kuwa **Lemutuz Online TV** haitarudia tena kutenda kosa.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Lemutuz Online TV** imefanya kosa la kuchapisha maudhui yasiyofaa mtandaoni na kushindwa kuonesha weledi kwa kutozingatia Sheria, Kanuni, na Maadili ya uandishi wa habari;

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa Mmiliki wa **Lemutuz Online TV** kuwa siku ya tukio alikuwa hospitali hauna msingi kwa sababu alishindwa kuimarisha mifumo ya usimamizi. Vile vile alipotoka hospitali alishindwa kusimamia na kuangalia kilichokuwa kinachapishwa kwenye chaneli yake na badala yake alikwenda TBC kuhamasisha watu wengine wasichapishe picha kama hizo;

6.3 Pia, Kamati imeona kuwa utetezi wa **Lemutuz Online TV** kuwa mwandishi aliyechapisha picha na video hakujua kama lile ni kosa sio wa msingi kwa sababu ujinga wa sheria sio utetezi (ignorance of law is not a defence);

6.4 Kamati imeona kuwa **Lemutuz Online TV** walichelewa kuziondoa picha na video zisizofaa kwenye chaneli yao na pia kuonesha kutowajibika pale ambapo wakati shauri likisikilizwa, Bw Malecela alisikika akimuuliza msaidizi wake iwapo picha hizo zimeondolewa au la;

6.5 Hata hivyo, Kamati imetilia maanani ushirikiano waliouonesha **Lemutuz Online TV** kwa kukiri kosa lao, kuomba radhi, na kuahidi kutorudia kosa lililopelekea kufika kwao mbele ya Kamati.

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA LEMUTUZ ONLINE TV

Kamati ina lengo la kuimarisha fani ya utangazaji na kamwe haina nia ya kubana au kuzuia ubunifu wa watangazaji, bali inawataka watangazaji kuboresha kazi zao kwa kuandaa na kutangaza maudhui yanayozingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya fani ya uandishi na utangazaji wa habari nchini.

Hata hivyo kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Lemutuz Online TV** yafuatayo;

Kuimarisha usimamizi makini wa chaneli yao ili kuhakikisha kuwa maudhui yao ni salama kisheria kabla ya kuwekwa mtandaoni. Hatua hiyo itaiwezesha Lemutuz Online TV kuepuka kuvunja sheria na Kanuni za nchi.

Kuajiri wafanyakazi wenye taaluma ya uandishi wa habari, kuwafuatilia na kuendelea kuwajengea uwezo zaidi ili waweze kuzingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari katika kazi zao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Lemutuz Online TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Lemutuz Online TV** kupitia chaneli yake mtandaoni imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa **Lemutuz Online TV**;

1. **Wanapewa Onyo Kali**;
2. **Kuomba radhi kwa Watazamaji** kupitia chaneli yake kwa kosa lililofanyika kupitia chaneli yao iliyotumika kutendea kosa kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia tarehe 04 Septemba, 2019.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **03** mwezi **Septemba** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeinengo-Sia Msoka**

.......................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ..................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**..................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**..................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**..................................